

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

**KINANGOP CONSTITUENCY, HELD AT NJABINI CHIEF'S CAMP,
KINANGOP**

ON

APRIL 17, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, KINANGOP CONSTITUENCY AT NJAMBINI CHIEF'S CAMP ON
WEDNESDAY, 17 APRIL, 2002.**

Present:

Bishop Bernard Njoroge Kariuki - Commissioner
Prof. Wanjiku Kabira - "
Mr. Paul Musili Wambua - "

District Officer

Secretariat staff in attendance:

Roselyne Nyamato	-	Program Officer
Jacklyne Obiero	-	Assistant Program Officer.
Regina Mwachi	-	Verbatim Recorder.
John Njuguna Gikonyo	-	District Co-ordinator.
Aggrey Akaranga	-	Sign Language Translator

The meeting was called to order at 10:00 a.m.

The District Coordinator welcomed the Commissioners and gave the opening remarks of the meeting for the day.

Commissioner Bishop Bernard Njoroge spoke briefly, and then he handed over to Commissioner Wanjiku Kabira. She gave the formality of how the hearings will be conducted, and then handed over to Commissioner Wambua to greet the people and to run the rest of the meeting.

D.O: ...Mkutano wa siku ya Leo, on time tena, najua wametoka mbali, barabara zetu ni mbovu, tena nao wamekuja na, sijui ni baraka au ni namna gani? Naona tangu asubuhi mvua imekuwa ni nyingi sana, kwa hivyo tunajua ni baraka wametuletea. Ni kuwakaribisha tu katika eneo hili la South Kinangop, na kwa niaba ya watu wa Kinangop, ninawauliza mjisikie huru pamoja nasi. Pamoja na hayo tunawahakikishia kuwa wakati tunaendelea, ni mvua tu ndio inatuzuia lakini watu wa Kinangop wako na hamu sana kutoa maoni yao kuhusu Katiba na mabadiliko ya Katiba. Sasa ningependa kuwashukuru wananchi kwa kujitokeza kwa wingi ili mtoe maoni yenu. Nadhani sitasema mengi kwa sababu kuna wataalamu hapa.

Lakini kile nitasema tu, mkutano wa leo madhumuni yake ni ya maana sana, kwa siku zijazo kwa nchi yetu. Kwa hivyo, kile nitaomba wakati ambapo mnapochangia, muwe mnaweka tu maanani zaidi kuwa ni Kenya ya aina gani ambayo tunataka vizazi vyetu virithi kwa siku za usoni. Kwa sababu, Katiba ni sheria kubwa katika nchi, na ndio kama mwongozo wa nchi itaenda namna gani na itatawaliwa vipi. Kwa hivyo, yale maoni yote ambayo mnatoa yatachangia katika mwelekeo ambao nchi yetu itachukua.

Sitakuwa na mengi sana kwa sababu Commissioners wako na programme yao, na kuna utaratibu ambao watafuata, nikuwakaribisha tu pande zote katika kikao hiki. Kwa hayo machache nadhani nitarudishia bwana Bishop na kuwauliza muwe huru kutoa maoni yenu. Nikidhani leo Commission iko hapa, hawajapanga safari nyingi, kwa hivyo mtoe, hata ile ingine, - unajua wazee wengine wanakuwa wataalamu wakiwa kule nje, pengine wakiingia hapa, huo utalamu, ama sijui pengine wakiona au kusikia Commissioners wako hapa wataingwiwa na uoga sana, waseme yale mapendekezo yao hayatatiliwa maanani sana, - toa yote, hata kama unaona pengine hauna uhakika nao, kuna wataalamu wataenda kuchambua na pengine wataandika vizuri kidogo kushinda yale maoni ulikuwa nayo. Kwa hayo machache, karibuni Commissioners, katika South Kinangop division, na mtatuongoza katika sehemu iliyosalia, bwana Bishop karibu.

(Clapping).

Com. Bishop Njoroge: Ahsante sana bwana D.O. kwa kutukaribisha, na tunawahakikishia mtoe maoni yenu bila uoga wowote. Hayo ni mawazo mazuri kutoka kwa bwana D.O. na kwa hivyo hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kuogopa kuongea na tuko tayari kabisa. Ningetaka kuwafahamisha kwamba siku ya leo tumekuja kwa ajili, - ama Commissioners wamekuja kwa ajili ya kupokea maoni kwa sababu ya Katiba -. Ni vizuri tuelewe hivyo kwa sababu mara nyingi tumekuwa tukizunguka hapa Kinangop Constituency, kwa sababu ya civic education, kufunza watu, ili wajiandae kwa ajili ya kutoa maoni. Watu wamekuwa wakitoa maoni wakati ambao haukuwa wa kutoa maoni, lakini leo ni siku ya kutoa maoni, ni vizuri tujifafanue vizuri, leo sio siku ya kusomesha watu, ni siku ya kutoa maoni, kwa hivyo msidhani kwamba ni ile mikutano mingine tumekuwa nayo ya kufunza watu.

Tuko tayari kupokea maoni kutoka- kama vile nimeona wengine wameandika kwa makaratasi- the Commissioners wako tayari kupokea, - wengine wako tayari kuongea- mtu mmoja ameniambia “mimi nataka kuongea sitaki kutoa makaratasi,”- ndio, mtu ako huru kuongea ama kutoa karatasi, ama kama bado kuna wale wamefika kile kiwango cha juu cha technology ya computer pia views zenu zitapokelewa. Hali ile yeyote ambayo maoni yako yako, uko huru kutoa maoni yako. Kunaweza kuwa na wengine kati yetu ambao wako na shida, wanaweza kuwa na shida ya kuongea Kiswahili ama Kiingereza. Ongea lugha yoyote ile, ambayo unaweza kujieleza vizuri. Kuna watu ambao watakalimani lugha ile utatumia. Kama wewe unajua Kikuyu ndio unaweza kutumia, basi ongea Kikuyu, tutatafsiri.

Nafikiri kwa hayo, sasa tutataka kuwakabidhi Commissioners watueleze. Okay, ahsante. Nimekumbushwa ya kwamba hatuna haraka. Kama vile bwana D.O. amesema, ni siku ya kutoa maoni, hatuna haraka. Tumepanga kumaliza mkutano wetu saa kumi na moja, lakini sisi ni watu ambao tunaweza kuangalia tuone watu watakuwa wamefika wapi, tuone kama tunaweza kuongeza muda mwingine. Lakini pia tumebarikiwa sana hapa kwetu Kinangop, kwa sababu hata kama hatutaweza kuwasilisha maoni yetu hapa leo, kesho tuko Engineer, na ni karibu tu, kwa hivyo tumebarikiwa sana, tuko na nafasi mbili ya kutoa maoni yetu, unaweza tolea hapa leo, ama kule Engineer kesho. Kama una rafiki yeyote ambaye ulisikia akisema, alitaka kutoa maoni na akachelewa, basi mwambie ana nafasi nyingine kesho kule Engineer mchana wote, lakini leo tuko hapa mpaka saa kumi na moja na kama kutakuwa na haja ama sababu tutaongea tuone vile tunaweza kuongeza huo muda. Kwa hivyo, karibu.

Com. Kabira: Habari za asubuhi! (Speaks in kikuyu), translation: nitamuuliza Commissioner Wambua awasalimie, halafu tutaanza. Vile tutafanya Com. Wambua akisha wasalimia, yule atazungumza atakuja hapa na atapatiwa microphone, awaangalie na atuangalie, halafu kuna mtu mwingine hapo, huyu madam mnaona ana machine, tuta record na mwingine hapa ataandika. Kwa hivyo maoni ikiwa mmezungumza itawekwa kwa cassette, na mkiwa na maandishi, mtapeleka huko ukimaliza, halafu utaandika jina lako na u-sign kuwa umetupatia hayo maoni. Ahsante! Nitampatia Com. Wambua.

Com. Wambua: Hamjambo! (Answer: hatujambo). Hamjambo tena,(answer: hatujambo)-

(Interjection)

Kwa hivyo tungelipenda kuanza sasa, na kama mlivyoelezwa, mnaweza kuzungumza tu ama unaweza kupatiana maoni yako kama yameandikwa, na kawaida vile tutafanya kama unatupatia memorandum ama maandishi, tutakupatia muda tu utueleze kwa kifupi maneno ambayo uliandika hapo. Kama unataka kutoa maoni bila kuwa na ouncilor ama maandishi, basi tutakupatia muda zaidi. Kawaida huwa tunapatia kama dakika kumi. Kwa hivyo, tungelipenda kuanza na yule aliyefika kwanza, na tutafuata taratibu hizo tu. Yule alifika kwanza tutaanza naye. Kwa hivyo tuanze na –first come first heard-aliyefika kwanza tutamsikiza kwanza, halafu tufuate hiyo list.

Kwa hivyo naweza kumwita aje hapa mbele, na ukifika hapa tafadhali utatueleza jina lako ni nani, unafanya kazi gani, halafu unatoa maoni, maanake tunataka ku-

(Interjection)

tunaanza na John Kihoro... utatuambia jina kwa kurecord halafu utatuambia... kazi gani unafanya, halafu utoe maoni. Na tafadhali kama ni oral presentation ama kuzungumza bila memorandum tutakupatia muda wa dakika kumi, utueleze kwa kifupi, usipanue sana, halafu mtu yule anaye fuata, unaweza kuanza bwana Kihoro.

John Kihoro: Ahsante sana Commissioners na watu ambao tuko hapa. Mimi ni John Kihoro na ni Chairman wa chama cha Ford- People katika sehemu hii yetu ya Nyandarua kusini. Mimi ningetaka – jambo la kwanza, tumekuwa katika nchi hii kwa muda mrefu, wa vyama. Na vyama vimekuwa vikinyanyasa watu, kwa sababu, lazima ukitaka kusimama kiti kama ni cha Bunge, ama cha udiwani unaambiwa ni lazima uwe wa chama fulani.

Na ukiaangalia hivi vyama, vyama vinaonekana ya kwamba vingine vinanyanyasa watu sana. Vinakuwa ni kama vyama vya watu, kama kampuni za watu, na hiyo mimi ningependa kuwe na indepent candidates. Iwe katika sheria ya Kenya. Hata kama kutakuwa na vyama vingapi ama vingapi lakini pia kuwe na independent candidates, ambao kama wanajijua wanaweza kusimama katika sehemu yao, kwa sababu wakubwa wengine wanasema “huyu asikubaliwe na asipewe clearance ya kusimama na chama fulani.” Hilo ndilo jambo langu la kwanza ambalo ningependa nchi yetu sasa iweke katika Katiba, lazima tuwe na independent candidates.

Jambo la pili ambalo ningetaka hii nchi yetu iwe, - tunasema ni nchi ya watu. –na hii ni masikizano ya wanaotawaliwa na wanaotawala. Kama ni hivyo, sioni ni kwa nini sheria zinatengenezwa na zikifanya kazi raia au watu wenyewe hawana nafasi ya kusema mwisho. Na ndio ningetaka katika sheria ambazo zitakuja kuwe na referendum. ‘Maoni yetu’, -hata kama hatujasoma, ikiwa pamoja na ya wale wamesoma, wataalamu wanaweza kuwa na mjadala ambao, tunaona wale wabunge ama wale watu wakubwa katika nchi, wanafanya jambo ambalo si la haki, likiletwa kwetu tuambiwe tuseme “yes/no, yes/ no,” sisi raia. Sisi tunaolewa ya kwamba hilo jambo ni letu, si la wakubwa wenyewe, na wakitaka kugeuza jambo hata sisi raia tuwe na nafasi ya

kusema.

Jambo la tatu ambalo ningetaka Katiba iweke, ni ya kwamba, tumefanya kazi, -kuna departments za serikali- na departments zingine ukienda kupeleka jambo, husikizwi. Na kwa sababu husikizwi, nilikuwa nikitarajia tuwe na ofisi ambayo, hata kama wewe ni wa department hiyo uwe ukipeleka malalamiko yako. Ile ofisi nasema ni ya 'ombudsman,' mahali ambapo, hata kama sijasoma, hata kama sisikizwi na department fulani naenda huko, huyo mtu anajibu na kusema ya kwamba hii ni complaint.

Na jambo la nne ni hii habari ya Local Authorities. Tumekuwa na local authorities katika nchi yetu, ambazo zinaokota pesa, na vile hizi pesa zinaokotwa, vile zinatumiwa, huwezi kujua wale walitoa kama ni watu wa maduka, kama ni wa nini, unaona huko hakuna kitu. Kwa mfano zamani tulikuwa tukiona local authorities inaleta pipa ya takataka, na hiyo takataka ikijazwa hapo inakuja inachukuliwa. Lakini siku hizi unaona Local Authorities ziko ambazo huelewi zinafanya nini. Kwa hivyo kama ni Local Authority katika sehemu fulani, lazima zipewe uwezo fulani. Kwa mfano, zamani local authorities zilikuwa zikiangalia elimu, zilikuwa zikiangalia hospitali katika sehemu zao. Lakini siku hizi inasemekana ni mambo ya serikali kuu.

Na hii serikali kuu inasemekana ni serikali kuu, unaona mahali pengine kama ni hospitali hakuna madawa, kama ni shule, hakuna waalimu wa kutosha, unaweza kuona darasa moja lina wanafunzi sitini au thamanini na mwalimu ni mmoja, na inasemekana ni shule ya serikali. Kwa hivyo, hiyo ningependelea kama ni Local Authority, katika mahali wanakaa, wapewe uwezo juu ya hiyo elimu na pia health services.

Na jambo langu la tano, nataka kusema ya kwamba, watu hawa wakubwa, (Pause) – okay-, nataka kusema, National leaders kama President ama yule ambaye anapatiwa mamlaka, asiwe,- ikisemekana kama vile tumekuwa tukiambiwa kwa miaka hii yote imekwisha, tunaambiwa ati mtu ni above the law. Huyu mtu ambaye anakuwa above the law, -hata unaona kwa mfano, mimi nimekuwa Chief- unaskia unaambiwa ati kuna sheria imetoka juu, huwezi kujua kama ni ya D.O. huwezi kujua kama ni ya D.C. huwezi kujua ni ya nani, unaambiwa lazima uongee hiyo sheria kutoka juu. Basi kama kuna viongozi wa nchi, ambao wanasemekana ya kwamba ati wako above the law, hiyo isikubaliwe. Katiba ambayo mnataka kutengeneza hii, kusiwe kuna mtu ambaye ako juu ya sheria. Kila mmoja akifanya makosa, kama ni President, kama ni Councilor, kama ni Chief, kama ni nani, ashitakiwe na kusiwe na mapendeleo. Kwa hivyo 'above the law' hiyo mkatae kabisa.

Jambo langu la sita: ni hii habari ya pesa ya nchi. Naona, kwa mfano hii pesa ya nchi yetu, wakati wa kwanza ilikuwa na kichwa ya President Kenyatta, sasa ina kichwa ya Moi, je, Moi ataondoka, sasa, tena itakuwa na kichwa ya President mwingine? Kwa hivyo inakuwa kila wakati pesa ikija inakuwa ni ya mtu, badala ya kuwa ya nchi. Na ningependelea kama ikiwezekana, pesa ziwe zinaonyesha nchi yetu.

Kwa mfano sisi tuna mlima hapa ambao unaitwa Aberdare, kule maji ya Nairobi inatoka, si basi pesa zetu zingine ziwe na Aberdare? Zingine ziwe na Giraffes, zingine ziwe na (Inaudible), badala kila wakati ukiongea zinaonekana hizi pesa ni za Mtu ukiongea unasema hii pesa ni ya Moi, hii pesa ni ya Kenyatta, na Kenyatta sio nchi, Moi sio nchi, pesa ni ya Kenya. Basi kuwe na pesa ambazo zinaonyesha alama ya nchi na sio alama ya mtu.

Yangu ya mwisho ni hii habari ya brutality ya polisi. Inaonekana- mimi nimekuwa mwana siasa – juzi tulipokuwa tukifanya mikutano ya 97, ilisemekana kuna I.P.P.G. ambayo ilisemekana ati watu wakiwa wanataka kufanya mikutano, inasemekana waende police. Juzi naenda police, tukija hapa tunafukuzwa na watu wa K.A.N.U. hawafukuzwi, unaona Chief anafukuza sisi watu wa Opposition, anafukuza watu wa vyama vingine na yet, hawa watu wengine hawaulizwi.

Nasema hii brutality, hata hawa watu wanasema ati wanafanya kesi, wanasaidia chama, kuwe na sheria ambayo, hata kama kunakuwa na President, hata kama ni nani, watu wa administration wasiwe kama youth wingers wa President. Wakubaliwe wawe ma-officer, ni watu qualified, wameenda course, wasiwe youth wingers wa serikali. Wawe watu wa kusema kama ni orders, watolewe orders za watu wote. Kwa sababu kuna wakristo, kuna makafiri, kuna waislamu, lakini inaonekana tu kama ni hiyo habari ya kufanya mikutano, inaonekana kama mkutano ni wa K.A.N.U. tu, ama chama kinachotawala, hao wengine si kama watu. Wanafukuzwa, tunawekwa cell, tunalala huko, hayo mambo yafupishwe kabisa na yasikubaliwe. Kwa hayo ningesema nimefikisha ile ambayo nilikuwa nimetayarisha, na nasema ni shukurani nafikiria nimeweka sawasawa.

Com. Wambua: Ahsante sana bwana Kihoro. Wale ambao watakaomfuata wafuate mfano huo huo, kwani amechukua dakika kumi kamili. Kwa hivyo, swali moja tu Bwana Kihoro; haya maswala ambayo unataka yapelekwe kwa referendum, ni maswala yote au kuna maswala fulani?

John Kihoro: Kuna maswala, kwa mfano, wabunge wanaenda bunge, kuna mahali wanasema wanataka 75%, na unasikia vilevile wanashindana, inasemekana hata hawakubaliani, inakuwa ni Presidential, anatoa kitu kama decree, badala ya hiyo, kama wamekosana huko, badala ya kung'ang'ana na wanang'ang'ana kwa sababu ya sheria yetu, hiyo maneno iletwe kwetu, sisi tujiamulie. Tubebe msalaba wetu. Lakini watu mia mbili wanatukatia jambo watu milioni thelethini au milioni kumi, tunaumia kwa sababu ya selfishness ya watu mia mbili.

Com. Wambua: Ahsante sana bwana kihoro. Mtu atakayefuata ni Father Kiarie.

(Interjection).

Com. Wambua: Kuna – nafikiria kuna memorandum ambayo itatolewa hapo na... sijui jina lake, lakini kwa niaba ya Father Kiarie, kwa hivyo unaweza kuja hapa mbele tafadhali halafu utueleze memorandum iko na nini. Uko na nafasi tu ya Highlights pekee yake, kwa sababu huwezi kusoma hiyo memorandum yote. Una dakika tano pekee yake.

Paul Munyuiru: Jina langu ni Paul Munyuiru kutoka shule ya parokia ya Njabini Catholic church, ambayo ina watu elfu tano mia sita. Mambo ambayo tumeyategemea au tumeangalia – I think I should use English, it's faster-okay we have the preambles and this is: that the constitution be made by the people of Kenya, the people of Kenya are sovereign, no law or authorities above the people, Kenyans are committed to democratic values of constitutionalism, equality and the rule of law. Kenyans are committed

to the future of Kenya, as a united and indivisible country and composed of people of diverse culture, whose rights are easily inviolable, the language of the constitution should be simple to be understood by the Kenyan people.

Exceptions to rights should only be coming by where 'several rights conflict,' then we need the direct principles of the state policy.

One: On National philosophy and guiding principles, Gender equality and protection of rights, of the minority are elements of a just society, all the political regions of the country are entitled to equal development. Children, young people, the elderly, and other vulnerable groups should be protected. Traditional customs should be guide lights in the society, provided they do not harm any sector of the society. Of particular importance would be the formation of village councils of elders.

Democratic principles: All belong to the people and are exercised on behalf through representatives, sensitive and accountable institutions of governance. Constituency and the rule of law must be adhered to. All human beings are equally entitled to civil, political, economical, social, cultural and developmental rights. Natural resources belong to all citizens. The natural environment must be protected. Citizens have the right to associate without any hindrance.

Constitutional Supremacy: On constitutional change the constitution must indicate that in the event of overhauling the constitution, all Kenyans shall be involved. In the event of the amendments, these shall be subject to a referendum before they are enacted by Parliament. This will keep Kenyans abreast with hitherto development in their constitution.

Human Rights: Every Kenyan shall be guaranteed food, shelter, clean water security health care education and employment. Every Kenyan shall be entitled to social, economic, political and cultural development. Primary school education should be made compulsory and free for all Kenyans. Secondary and University education should be accessible to the poor, the bright, young people. All workers should be guaranteed the rights to Trade Unions representation. Capital punishment and torture should be outlawed. Kenyans should be guaranteed the freedom of movement association and expression. An independent Human Rights Commission should be established. The Director of this Commission must be accorded security of tenure. Minority and underprivileged handicapped and aged, rights must be guaranteed.

Citizenship: All people born in Kenya of parents who are both Kenyans, all children born outside Kenya, of parents who are both Kenyan citizens, all children born of one Kenyan parent, regardless of gender, spouses of Kenyan citizens, regardless of gender must be entitled to automatic citizenship even when they are citizens of their own countries. The constitution should allow dual citizenship. Missionaries should be exempted from any form of taxation.

Land and Property ownership: The government should have power to compulsorily acquire private land for purpose of development of social amenities e.g. roads, hospitals schools, extraction of minerals, for the purpose of the country's development. The owners must be fairly compensated and promptly. The Ministry of Local Authority should have power to

control the use of land. The government should reclaim big chunks of land that are not put into proper use for economic development. There should be a ceiling of acreage of land owned by individuals, and the issue of squatters be addressed.

Men and women should have equal access to land and property ownership. Kenyans should have constitutional rights to own land and property entitled in any part of the country.

Government: Parliamentary government should be adopted. Real power of the government should lie in the Parliament. The Legislature has Supreme Authority. Parliament should appoint a prime minister from majority party to be in charge of the daily running of the government and directly accountable to parliament. There should be, independent three arms of government, there should be absolute separation of power reinforced by operational checks and balances.

The Executive: Qualities of a President: - must be born in Kenya, Have a degree of prevalence, education, sound mind and good conduct, integrity, economically stable, and should declare wealth. Age should be 35 to 60 years, no criminal record and of course must be married and with a stable family.

Powers: Appoint Ministers and constitutional officers, after being vetted and approved by the Parliament, run government affairs as approved by the Parliament, two years term of office-five years each. Cabinet Ministers must not be drawn from members of Parliament, - that is separation of power-, cabinet should be answerable to parliament, Prime Ministers must attend Parliament and answer questions, the Chief Executive can be removed from power by Parliament- the Legislature-, be above 30 years of age, have at least a Diploma, no gender discrimination or handicaps, no criminal record, be a resident of the constituency. The constituents must be empowered by the constitution to recall their M.P.s in the event that they are not satisfied with his or her representation or performance. This should be done through collection of 1,000 signatures across the constituency, registering people's disqualifications.

Powers: Parliament should vet the appointment of Ministers, assistant Ministers to make the ministries more professional and accountable, court judges through parliamentary judicial Commission.

Public service Commission officers:

Interjection (In the background: 'time is running out.').

Okay, since time is running out, we have also taken into consideration the use of natural resources to all through out the country, the electoral process must also be fair and free, all political parties should be registered and be guaranteed operation and be funded from the ex-chequer, Commissions of inquiry should be formed by Parliament and clear findings be given to the Kenyans, Civil and public education should be given to all Kenyans.

We also have concerns where we have conflicting views, they should be carried out to a National referendum, and this memorandum was compiled by twenty two participants after collection of their views, the parish priest was in charge, we had the seminarians, we had two sisters, people from catholic justice and peace Commission, C.W.A. that is catholic women association, catholic men association were there, we had choir representatives, we had youth, we had people who are disabled, we also had single parents.

Thank you.

Com. Wambua: Register the memorandum there, and it will be accepted.

(Com. Prof. Wanjiku speaking from the background, not clear.)

Com. Wambua: Kuna mtu ambaye hawezi kuelewa Kiingereza hapa?

(Answer: wengi.)

Com. Wambua: Wengi. Hamukusikia mambo ambayo yalizungumzwa hapa?

(Hatukusikia).

Com. Wambua: Basi wale ambao watazungumza kwa Kiingereza, na wale ambao wataleta maandishi hapa ikiwa na maoni yao, tutajaribu kwa kifupi tu, kutafsiri yale ambayo watakayo sema. Kwa hivyo msiwe na shaka ati hamuelewi kitu gani kinasungumzwa hapa, tutapanga huo mpango. Lakini tutaendelea. Tumwite bwana Joseph Mbatia. Joseph Mbatia yuko wapi?

Interjection.

From the background: Mbatia alikuwa hapa mbeleni, lakini ameniwachia memorandum yake.

Question: Imeandikwa kwa Kiswahili?

Answer: Imeandikwa kwa Kiingereza.

Question: Na alikwambia ufanye nini?

Answer: Aliniambia nikupatie.

Question: Kwa hivyo hataki kuzungumzia mambo yake?

Answer: Eee, aliniambia tu niwapatie. Lakini ni mimi namba mbili nafuata yeye, nitasoma yangu.

Question: Hii ni gani?

Answer: Hii ni ya Mbatia.

Question: Na wewe ni nani?

Answer: Mimi ni Gachomba.

Com. Wanjiku: What you do, just put it there. Read yours bwana Gachomba.

Gachomba: Ahsante sana bwana Commissioners, na watu wale tuko nao hapa, wote nawasalimu. Yangu nitagusia sana mambo ya Human Rights. Na zile niko nazo hapa kidogo ni guarantee...

Interjection

Com. Wambua: Mnaelewa hio lugha?

(Kidogo)

Gachomba: Guarantee the citizens Human Rights. Nitaweza ongea kidogo juu yake kwa Kiingereza vile nimeandika hapa. In the new constitution the government should recognize the role of Human Rights in the maintenance of self respecting and Nation capable of charting out her own course of development, convinced that the pursuit of basic Human Rights is a responsibility of all democratic forces and aware that such rights have in the past been abused.

Interjection.

Com. Wambua: Which language do you want to use?

Gachomba: Ile nimeandika tu hapa.

Com. Wambua: umeandika kwa Kiingereza?

Okay what I was saying is that we have to observe, in observance we get the policies of Human Rights that the government should at least uphold at all costs. Sasa nitaanzia namba moja:

- ◆ Right to life and security of person.
- ◆ Right to food, clothing, shelter and medical Equipment.

Interjection.

- ◆ Treatment

(Interruption from behind)

- ◆ Treatment, education, culture, social security, must all people have.
- ◆ Right to privacy of ones home, property and possessions.
- ◆ Right of academic freedom, of schools and universities.
- ◆ Right to enter, remain and leave the country.
- ◆ Right to passport and general respect of our citizenship.

Right to opposition, demonstration and petition for redress of grievances

- ◆ Rights to freedom of movement and residence in any part of Kenya.
- ◆ Right to freedom of assembly and meetings
- ◆ Right to freedom of trade and occupation.
- ◆ Right to a healthy environment
- ◆ Right to have and own property in any part of Kenya.
- ◆ Right to have proper fair and good behavior of government officials, and
- ◆ Right to fair and free, right review process of the Law.

That should be the government's common pledge to all Kenyans.

Hapo nitawachia hapo kidogo, niongee mambo sasa ya vile Commissioners sasa mmeingia kwetu tunatoa views ambazo ni Katiba ambayo tunaweza tengeneza ya watu wetu ya miaka kama mia mbili inayokuja, sivyo? Mimi ningependa kuuliza, sababu tumekusanyika hapa sisi wote, Wakenya, will there be anybody who will tamper with this constitution because after that mnaenda kupeleka hii makaratasi pahali pengine, will they be interfered with? Now lazima mtuambie kwa sababu hata wa leo ...

Interjection. (From the Commissioners): Just a minute, are you asking us questions or giving your views? Kwa hiyo maswali ambayo umetuuliza, tupatie maoni yako, just give us your views stop asking questions.

Gachomba: Okay, haya maoni natoa ndio nasema iwe respected, na kwa vile nimeyatoa, isiwe nikusema tu na mdomo. Kwa sababu hata ile Katiba tuko nayo inatuonyesha ukweli, wazi wazi kama vile nilivyo soma hapa, - ‘You can own property anywhere in this country’.- Lakini tukiangalia sanasana kama wale watu wakutoka huko Molo walipigwa juzi na tuko na sheria ambayo tayari imesema “we have to own that property.” It is in the constitution. Ndio maana nina sema kwamba in future if this constitution shall not be tampered with, we shall be very happy. And if it is tampered with, then there is no constitution making here.

Thank you sir.

Com. Wambua: We have noted that. Only one clarification to be made here. Are you talking about the new constitution or the old one?

Gachomba: In the new constitution. In the past the constitutions have been tampered with.

Com. Wambua: Okay register ile ya bwana mbatia, akija, akipenda kuzungumza machache juu ya memorandum yake, tutamruhusu. Okay, we proceed, tutaita Peter...

Interjection: *Aria mataiguaga Githungu, maundu maria mamwe ahutia ni wiyani wa muoyo wa munddu na uwitir. Ahutia uhoro wa kugiana na maunde maria matuthiururikiirie marokorwa mari mega akorwo ni ta mai, akorwo maundu macio mari mega maikaire uria kwigiriire matikahutio. Akorwo ni ta ithaka mundu ni agie githaka o haria Kenya yaruma. Macio ni maundu ma mamwe maria agweta maria andika thiini wa memorandu.*

Com. Wambua: Thank you very much...thank you very much... Peter Kibe Kang’ethe.

Peter Kibe Kang’ethe: Okay, ahsante. Nina furaha kufika mahali hapa, na nitazungumza kwa Kiswahili kwa sababu nimeandika kwa Kiswahili, ingawaje mimi ni mkikuyu, lakini nitazungumza kwa Kiswahili, ndio tuweze kuelewana sote. Ninataka kuzungumzia – inaonekana watu wengi wa- Shida imekuwa sana katika serikali kuu, ama wale wamechukua nyadhifa za kiserikali, ndio maana tunagusia sana mambo ya kutoka Rais kuja chini, kwa maana ndio imekuwa ngumu kwetu, ingawaje tumekuwa na Katiba ambayo ni nzuri, lakini imekuwa imeshikwa vibaya. Sasa nataka kusema ya kwamba, nchi hii kama ilivyo, ni nchi ya kidemokrasia, na ni nchi ya wananchi, ni yetu. Sio nchi ya mtu binafsi ama kundi la watu. Hiyo ikae namna hiyo. Isiwe inakuwa captured na watu binafsi. Rais asiwe na uwakilisho wowote wa bunge. Hii ni kwa sababu sisi wafrika tuko na tegemeo ya kuwa mimi nikiwa Rais basi sisi watu wa Njabini stima zitakuja na hazikuweko, barabara zitatengenezwa na kulikuwa hakuna, yaani utajiri wote utarudi Njabini kwa sababu mimi natoka Njabini. Lingine, Rais anapaswa kuchaguliwa na wananchi kwa kura ya siri, na iwe ni asilimia 51%.

Kenya mzima awe na 51%, lakini sio awe amechaguliwa na kura 45% anaandikiwa President. Hata afadhali twende kwa duru ya pili. Akisha apishwa, Rais achague baraza la mawaziri wasio zidi kumi na watano. Na wizara zisizo zidi kumi na tano, na manaibu wasio zidi kumi na watano. Tumeona katika siku za usoni ama za nyumani, Rais anatuambia, oh, nimechagua mawaziri kumi na watano, wizara kumi na tano, mawaziri thelathini ama arobaini. Hii si mzuri, kama wizara ni kumi na tano, na nchi yetu ni nchi ndogo nchi masikini hakuna haja ya wizara nyingi. Wizara kumi na tano mawaziri kumi na watano manaibu kumi na watano. Okay, tena kuwe na parmanent secretary mmoja katika wizara, na huyo parmanent –hata kizungu na Kiswahili kinasema vizuri- parmanent secretary, huyo ni katibu wa kudumu. Sasa utakuta waziri anabadilishwa na P.S. anabadilishwa, hiyo ofisi inabaki nill. Inabaki empty handed, sasa kutakuja waziri mwingine na kuje P.S. mwingine, sasa wataanzia wapi? Hakuna mtu wa kumwambia mahali ataanzia mambo.

Okay, Rais kupendekeza baraza lake la mawaziri kwa bunge kwa muda wa siku saba baada ya Rais kuapishwa. Wabunge kuchagua makamu wa Rais kutoka kwa baraza la mawaziri. Hii ifanywe bila kuangalia chama, au makamu wa Rais apendekezwe na chama ambacho kina wabunge wengi bungeni, kwa sababu nchi yetu ni ya vyama vingi, kwa hivyo kuwe na uhuru wa watu wote wawe wanachangia katika serikali.

Wabunge kuwajaribu mawaziri kwa muda wa wiki tatu na kuwafanyia marekebisho. Marekebisho hayo, ni kwa sababu Rais anaweza kuchagua waziri ambaye hajasomea wizara ambayo anapewa, na wabunge wataenda wamjaribu- Mr Kibe, umepewa wizara ya elimu, je, umesoma? Je una elimu ya kutosha katika wizara hiyo? Utakuta mtu amepewa wizara ya afya, na yeye hata hajui madawa ni nini. Hata akipewa madawa anauza, kwa sababu hajui madawa ni nini, au ni ya nini. Kwa hivyo, Bunge iwe iko na uwezo wa kumjadili huyo mtu kama anaweza kazi hiyo ama hawezi. Kama hawezi, Rais anaambiwa kwamba ondoa huyu tulettee mtu mwingine.

Okay, Rais awe mwajibikaji. Kuajibika kazini. Akiwa kazini awe huyo mtu-, ni kumuajiri tumemuajiri, sio yeye ametuajiri. – Kwa hivyo awe mwajibikaji kazini, akiwa katika ofisi hiyo afanye kazi kama mwajiriwa sio kama ofisi ni yake. Awe anafanya kazi yetu – mwajibikaji-.Kitu kama akiharibu jambo fulani, Rais awe akishtakiwa, kama atapatikana na makosa; na asiwe juu ya sheria- above the law-.Kwa sababu hiyo ndio kitu inatusumbua, hata Rais hawezi kuwa mwajibikaji katika Kenya. Kwanza hiyo tukikataa kubadilisha, katika siku za usoni, Kenya haitakuwa na Rais ambaye ni mwajibikaji.

Kwa sababu yeye yuko above the law atakuwa *ana-violate* kila kitu. Mambo mnayompa afanye yeye anafanya vile anataka, sio vile nyinyi mnataka. Mkimpeleka kotini, hiyo inatupiliwa mbali. Sasa nakuja kwa mambo juu ya mkuu wa sheria. Na hii ndiyo ya mahakama na ndio imeleta shida katika hii nchi yetu. Achaguliwe na Bunge na awe mwana sheria, asiwe rafiki wa mtu yeyote aliyefikishwa mahakamani. Kisheria, mhalifu atangazwe kuwa huyo mtu ni mhalifu. Sijui kama ndivyo ilivyo ama ni kuharibu wanaharibu katika sheria ya sasa, utakuta mkuu wa sheria anaenda kotini anasema “huyo mtu wachana naye.”

Umempeleka kotini, anatolewa polepole, polepole. Haya, ni makosa saa hii kuwa na waziri anayeitwa Kipng’eno arap Ng’eny.

Ni makosa makubwa sana. Kwa sababu huyu mtu ako na mashitaka kotini, na hakuna – ameshikiliwa tu na Rais – kwa sababu Rais yuko above the law, na huyo mtu yuko na mashtaka ya kuiba mamilioni ya pesa na bado huyo mtu ni waziri. Kama mtu ameshikwa na makosa, inafaa aondolewe. Kuna watu wengi wamesoma na hakuna kazi. Sasa nchi yetu inafaa iwe na sheria ambayo itasimamia kila kitu cha mwananchi. Mtu kama amefanya makosa anatolewa na anashtikiwa kotini. Na huyu mkuu wa sheria naye ahakikishe sheria zote zimetetelezwa na zimefuatwa. Na akifanya makosa – yeye mkuu wa sheria- yeye pia aondolewe. Kuwe iko body ya kumuondoa, sio tu mtu amewekwa hapo. Na ndio maana mambo yetu inaharibika kwa sababu kila kitu ni Rais, kumchagua- Rais, kumuondoa- Rais. Kama Rais hataki kumuondoa, hawezi kumuondoa.

Haya, awe mwajibikaji katika kuishauri serikali. Tumekuwa na wakuu wa sheria wengi katika nchi yetu ya Kenya. Na wamekuwa – kazi yao ni kupotosha serikali, - hawawezi kuambia serikali mambo ya ukweli kisheria. Akiwa kama mshauri wa serikali, anafaa awe mtu ambaye anaambia serikali-“hapa unaanguka,” “hapa unaenda vibaya, hapa unaenda vibaya”-, namna hiyo. Kule ambako serikali inaenda vizuri, anasema sasa tunaenda vizuri. Lakini tumekuwa na wakuu wa sheria wengi ambao ni wa kubandikwa, kubandikwa, kubandikwa. Awe akishtakiwa kama ako na makosa. Iwe iko body, akifanya kosa hata yeye aweze kushtakiwa. Haya nimekuja sasa makamu wa Rais na mawaziri na manaibu wa mawaziri. Wawe watu wasio na hatia ya ufiada ama uhalifu wowote. Siku hizi tumekuwa na mawaziri, manaibu ambao wako na record ya uhalifu lakini bado wako kazini. Watu ambao wanalingana na wizara wanazopewa – hiyo nilikuwa nimetaja-. Watu ambao ni waajibikaji kazini. Kazi ambayo wamepewa ikiharibika wawe wanashtakiwa kotini, na afungwe maisha.

Interjection

Makatibu na wafanyikazi wote wa serikali na mashirika ya serikali, hizo zote zisimamiwe na watu ambao ni waajibikaji kazini, na watu ambao wanalingana na wizara ambazo wanapewa. Kama vile nilikuwa nimesema, sio mtu kuokotwa tu huko anakuja anapewa kazi. Nayo upande wa utawala, from P.C. kuja hivi mpaka chief. Hiyo turudishiwe sisi wenyewe. Tunaletewa watu bogus! Watu wabaya. Hata huwezi kuenda kumuuliza swali. Turudishiwe sisi wenyewe, tuwe na uhuru wa kuwachagua. Nitamalizia hapo na jina langu ni Peter Kibe.

Com. Wambua Okay, tuendelee, na tutaita bwana Joseph Macharia.

Joseph Macharia: *Nii nigwaria na Gikuyu. Ritwa riakwa ni riu ndetwo Joseph Macharia, na ndoiga ngwaria na Gikuyu nitondu ona mahinda maria ndathiite murim, nithiite kinya Holland na ndariire na Gikuyu. Nekio riu gwaria na Gikuyu. Wa mbere ngwenda kugweta uhoro was kuma mwena wa na iguru. Kuma naigoro kuma kwari lights. Kyama kya mutogoria Rais amberirwe ni kuma thine wa bunge, na are thine wa bunge, thine wa Kenya ni kwaririwe ni kugea na kyama kigi. Dauga kukagia kyama igire kyama kya buge kana kyama gia kuma okodo profess modu omwe omwe nigetha Rais agiitokyo odo akaba rieta kyama kiu. Polytechnic hio ni ketha aitekeryo kana ni waothire thikari kana ni waothire da gorori. Todu odo dukaga niodo wa President atweka overall yaani dwigatweke President ni above*

the law. Toke mwena ene wa kutore coujoooni ni mwaka fulani itogoragia areo kuaka manyuba kushoka kuree planning thaine, todu nidarikana urya ndare murimo nidonire orya maigagia na guku thii na igerete madukaini ni tinyuba syabere gwako ni farafara yaberirwe kwejwa nyuba shyabirerwe kuakwa kwa ogwo ni plan ya birirwi.

Mwagana tudo ni uhoro wa migoda, kuri migoda megii ikaraga toho na gutiwira iritugarirwo na ado maikarite gishagi maitereri kou matere odu maikaga, kyogu migoda hiyo yatweke ya thirekari. Nigetha migoda ikarimwo tugatoma irio ulaya economy itige kuthoka. Ndwoke mweno wa agriculture, griculture matishoke kuikara mishye kwao maoke mogodaine makona wera huyu wararutwa nigetha makabuditya mudu wera ushyo tudo murimi aremaga rii na arimo atwari irimo shyake igatweka rimwe tijega todudare mudo amwonirie todumugriculture aikaraga gwake hata ginya ya ritwo. Ndike horo wa mwishi waiya ido shya modo na kumutunya, naonekane aika ogwo na igoti rine naika ogwo, mwishi wa kuiya ido shya ado kuiya na karamu, haiya ido shya thirikari tudo shyake ni shya ado dagashoke kuchejwa atwarwe ministry ige athie akaiye kwoo, mwishi ni mwishi atwarwe gotine ona akorwa ni President. Jike horo wa mikanya ya mwoshie, thine ya mikanya ya mwoshie maida matene anake matithakaga na hairetu hogu mathakaga nao na kumanyita na hinya. Kyogu agikorwa mudu murume ni awanyite mutumia na hinya hushyo ni arigwe ni kuitwo. Amenyekana fyo fyo hogwo digwo aigete. Ni maodo makwa mare kweda muno kueda kumaria kumakinya hau.

Translator:

Com. Wambua: Okay ahsante sana bwana Macharia, anayefuata ni bwana Zacharia Kimani.

(A question from the background- not clear).

Answer: Hapana tulieleza hapo tulipoanza, tunafuata taratibu ya majina ambayo imeandikwa hapa. Kama uliandikishwa kwanza wewe utakuja kwanza, kwa hivyo hakuna yule ambaye atafanya shortcut. Hii ni sheria ambayo tumeweka na tujue tutafuata hii hapa. Kwa hivyo msiseme kuna mtu alikuja na akapita. Na wale ambao bado wanataka kutoa maoni yao, register bado iko hapo kwa hivyo andikisheni majina yenu huko halafu tutaendelea kufuata majina vile yalivyoandikwa. Endelea bwana Zacharia Kimani.

Zacharia Kimani: Okay, ile mimi nataka kusema, the President should not be above the law, and the winning President should garner 51% of the popular votes on top of the 25% percent votes in five provinces. In case of no outright winner in the first round, a run off between the top two candidates should be held within twenty-one days. The President should not appoint top government officials e.g. Ambassadors, Heads of parastatals, so named. But should confer with parliament for the updating, which should have two-thirds majority.

The three arms of government should be (Inaudible) independent of each other. I support the abolishment of the provincial

administration, for it has proved to support the 'status quo'. I want devolving of power, but we should not adopt the Majimbo government. Rather, I prefer prime ministerial government, where we have a ceremonial President, with the Prime minister being the Executive, running the government affairs. I support the creation of an office of an ombudsman.

Eight, I want to support the calls for amendments, but it should be only after a redecision. In case of those who have stolen from public coffers, they should be made to pay, with interest at the current market rates.

I want to support the over hauling of the electoral Commission and appointment of non-partisan professionals e.g. lawyers, credit editing, and for... funding has been a problem to the electoral Commission. I suppose it should be independent of the ex-checkers. It should not be begging for money from the President or any other person.

The fundamental Human Rights as per the Bill of rights should be totally adhered to and severe punishment should be meted to any law offenders. Proper working conditions and remuneration to security forces in Kenya should be beefed up so as to beef up security. I am calling for the trial of those who committed crimes against (inaudible) of democracy in this country.

I support the funding of political parties from the ex-chequer, declaration of wealth by top government officials, land redistribution, and lastly, I want to support the division of national wealth.

You see there is this problem that if you do not support the current government, your infra-structure will be eroded and the rest. I am calling for-because; every Kenyan should pay taxes the national wealth should be shared equally. Okay, and the last, I want to – if the Commission can't be able to finish its work on time for the general election,- I'm calling for minimum reforms. Although there has been a problem on how these minimum reforms should be, but these minimum reforms should come from the people. The people should tell you the Commission how minimum the minimum reforms should be.

I have also said that we should go to the next general election with a new constitution, but the Parliament life should not be extended.

Thank you.

(Question from com. Wambua, not so clear)

Zacharia Kimani: I support the 'creation of a truth' and the model of that South-African truth and...

(Backed from behind)...

Yes.

Francis Maina: *Agweta maodo maya maria materaigwa gikuyu agweta ati Raisi ndagereru ni gukoro ari iguru wa watho, na gariro ni guthuro gicigo kia mlang tano na mwi hari igana kia miti uothe itketio hado ha githerino na ariga*

gukinyia kura ici na kugie na githurani gai kari masindine aria ari marakhanreri uria ukohoto atweke Raisi, naaria uhoro wa guthuro kwa anene a thirikali ambassadeurs, aria makearaga ma-office maria manene matigerero ni guthuro na Raisi we mwene. Na gwita huru wa kuneno kwa wa thani wa provinci kana kuna kweheria ate so Pc, DO, Chief ciothe cieherio, kugie na prime minister hado ha kugie na Raisi toguo tuwenake na kague na president wa guthiaga akoro ni university kwi na graduation gathi kouo, akoroa na bara bara arahikoro agithe kuo. president tucio na kugiye na office ya kurora mateta mandu. Agithikereria na koa ikinya. Na gwita uhoro wa aci uona maya indu cia mwingi kana therikali makreha indu icio na makareha na macioro. Gite gia kuhuia pesa kiogamirero budget agithomwo gikarutero mbeca gekanekero mbeca cia kuruta wira. Ogitere, kugie ni ogitere wa kugana niguo andu makoro magikara wega minathiyo.

Ciama cia siyaisa handu hakirugamerere kana agacariya jira ike cia gucaria mbeca hinde ya githurano budget agithomo ciama ciothe igakoro ifaikero ikaheo mbeca. Naya gwita uhoro wa kugaiono kwa utoka wa burori gutikagie na andu atoko na aria ake ni athini. Tondu githerino kihakuhe gekuhereriye na kitaba ino oriyo maoni aki kuru ni gukoro arikite githurano gegioka guthondikio Katiba ekihota guto twara githurano gike gigoko kwa ugo kogie na reform kana maundu maigana ona mekuguwanero nema magutotokoria thinia wa gethurana na giko ni reform iyo. Kana giko na Katiba njeru. Thank you.

Translator:

Florence: Hamjambo? Naitwa Florence, mimi ni mwanafunzi. First, it's about land. I think land should be fairly distributed, because there so many people who are landless, who even do not have anywhere to sleep and yet we have so much land in our country that is not used and so many people who own very large portions of land, which they do not even use.

Second, it's about security. We do not have security in our country today. For example, you cannot walk at night- you do not feel secure to walk at night and yet this is our country, and we should be secure in our own country. I think the government should provide enough security for everyone, and we should have freedom, because, in this country we have freedom and I think every citizen or every member of this country should have freedom to even walk at night, without being asked where you are going and where you are coming from. Because this is an independent country, I think people should have freedom to be at any place at any time, and there should be enough security for that person to be at that place at that particular time.

This being an agricultural country, I think that farmers should be protected from exploitation. Today, the farmers are doing a lot of work and things like fertilizers are very expensive, farm machineries are very expensive, and yet our products are being sold at very low prices. We, the farmers, are the ones who are suffering, and someone else somewhere is selling those products at very high prices. So I think the farmers should protected the government.

Third, it's about the people who govern us. For example the P.C., the D.C., and the D.O. We rely on these people, they rule us. So I think we should elect these people and not by someone else. Because these people are coming to deal with us, and it is us people who should elect them.

About the Vice President. I think that the Vice President is a very important person in our community today. He is a leader, and I think that he should be elected and not just appointed by one person, may be by the people, or the Parliament. Because he is a very important person in our community today, and it is us whom he leads. He is the next from the President and I think that we should elect him.

Lastly, there is so much harassment from the police today. You cannot walk maybe at night. Sometimes, may be you have done nothing wrong but you are being harassed. I think that the police should protect us people and not harass us, they should protect us and give us security and not harass us. That's all I had.

Thank you.

(Question from com. Wambua- not clear)

Florence: I think that everybody in our country should own land. May be it should be redistributed once more. And some land that is owned by the government should be distributed to the people.

Interjection. Com. Wambua asks questions and she answers.

(Translation for Florence in Kikuyu is done).

Com. Wambua Ahsante sana, tutamwita George Nga'nga. George Ng'ang'a.

George Ng'ang'a: My names are George Ng'ang'a, I will read my presentation. Our government – all public and government hospitals should be equipped with drugs and qualified doctors. Treatment should be made free to everybody. Doctors in government hospitals should be given a right to issue a person with P3 forms, instantly without consulting the police. And the forms should be kept in hospitals but not in police stations.

The other issue is about the councils. Councils should be made to account for the money they collect from the public. They take a lot and the public gains very little. They should erect public toilets, and...(inaudible) which should be in good shape.

The whole of the administration should be elected by the President, and they should serve at least for four or five years. The Kenyan currency should carry the picture of the current President.

The other issue is about security. Police patrols should be intensified, but harassment should come to an end. And then the regional policemen should be transferred to another station after serving for one year or two at most, to avoid being biased with overhauling cases. This is not an issue where the policeman stays for ten years at one station. His gunfires at...(inaudible) otherwise if he gets to know you, even your grandparents, you seem like friends.

Primary education should be made free and compulsory. The government should provide a way to take care of HIV/positive children unconditionally. That's my presentation.

Thank you.

Com. Wambua: Thank you very much. Translation please...

(Translation is done in Kikuyu)

Com. Wambua Thank you. Can we have Paul Ndumia?

Paul Ndumia: My name is Paul Ndumia Kariuki.

Interjection

Com. Wambua: Hiyo Dumia imetoka wapi?

Paul: Ndumia. (He then spells his name).

Laughter.

Paul: Okay, President should not be above the law. The Parliament but not the President should appoint the Vice President. The government has to give free hospitals and free education, because we are giving taxes to the government.

All the toll stations in Kenya have to be banned because toll stations are benefiting some people but not the government. The government has to take care of the forests, because people who are benefiting alone are stealing forests. The people who are benefiting from the forests are the foresters and the forest guards, because they are selling trees at low prices and the money is not for the government.

Number six: The police under the Kenyan government who will take bribes should be sacked. That is the presentation I have.

(Translation is done in Kikuyu).

Com. Wambua: We shall call the next, atakayefuata ni Jeremiah Muira. Jeremiah Muira Gatua.

